**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam**
**Tarehe 18 Agusti 2007**

**Waliohudhuria**
Ally Saidi Mohamedi
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Izdoly Aludo Kihalule
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Kassim Bakari
Mohamed S. Mwenguo
Mohamed Salum Athman
Mussa Athmani
Mussa Omari
Patrick Masinga
Saidi Hemed Mbaruku
Sosthenes C Amlima
Sudi Saidi Ramadhan

**Wageni**
Godfrey Jax – CHABADA
Selemani Majembele – AALOCOM

**Msafara wa baiskeli**
Mkutano wa msafara uliokuwa umepangwa saa tatu uliendelea kwenye mkutano mkuu. Wawakilishi wa CHABADA na AALOCOM walikaribishwa.

Juma aliarifu kuwa alipeleka barua za kuomba ufadhili kwenye Ubalozi wa china, Game shop – Mlimani City na Ultimate Security Paulo, Juma na Elaine walifuatilia Ubalozi wa Uholanzi siku ya Jumatatu. Elaine aliarifu kuwa amefuatilia kwa simu Bakhresa na Knight Support, lakini ilikuwa ngumu kupanga mkutano na watoa maamuzi na hapakuwa na ufadhili wowote wa fedha.

Elaine alisema kwamba bwana mjamba wa AALOCOM amemwambia kwa simu kwamba wametafuta ufadhili Barrick Gold, Coca Cola na Bakhresa. Selemani majembe wa AALOCOM alitakiwa kuthibitisha lakini alisema hakufahamu chochote. Ilielezwa kwamba AALOCOM inatakiwa ihudhurie vikao vya msafara ili tuweze kushirikiana kuomba ufadhili Barick Gold, kwani wao wanatuhumiwa kuua wachimbaji wadogo wadogo mgodini mara na kwamba wanaongoza kwa uharibifu wa mazingira na uvunaji wa haki za Binadamu. Jax alisema kwamba hakuna kampuni iliyo safi hivyo tutafute ufadhili kwao na kuwaeleza mawazo yetu. Elaine alimjibu kuwa kufanya hivi kutazuia sisi kuwakosoa na kwamba Barric gold nitofauti na kampuni nyingine. Alisema kuwa Mejah pia amekubaliana nae Jax alikubali kwamba kwa vile UWABA inaongoza jinsi ya kupata fedha kwa ajili ya msafara hiyo ilikuwa juu yao.

Juma alikumbusha kwamba mbunge wa Ilala amerudi Dar es Salaam. Alipiga simu na kupanga mkutano jumatatu itakayofuata. Asubuhi saa 3. ilikubalika kwamba tutahudhuria mkutano huu na kuendelea kufuatilia ufadhili kwa mashirika yaliyoko mjini – Bakhresa, Mohammed Enterprises na Ultimate Security. Jax na Majembele waliombwa pia kuhudhuria ili kuwakilisha mashirika yao. Walikubali kukutana na mbunge lakini hawatakuwa na muda wa kufuatilia ufadhili.

Elaine alimwambia Majembele wa AALOCOM kusaidia kukodi ukumbi wa Mnazi mmoja nae alikubali kufanya hivyo na Halmashauri ya Manispaa ya ilala au Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam, lakini akasema kwa vile bado miezi miwili kufika Octoba itafuatiliwa tena baadae.

Jax alipendekeza kuwa ana njia tofauti kwa wakati mmoja wa msafara.Elaine akakumbusha kwamba tuliandika pendekezo pamoja mwezi machi na lazima tutekeleze tulivyopanga Sosthenesss alipendekeza na ilikubalika kwamba ikiwa tutapata fedha zaidi tutabadili mipango lakini tukikosa basi tutafanya ilivyopangwa.

Kuna haja ya kuwa na mwenyekiti wa kamati ya msafara Jax alisema kwamba kwa vile CHABADA na AALOCOM wana mwakilishi mmoja mmoja kuwachagua itabidi iahirishwe hadi mkutano ujao

Jax alisema kwamba tutakutana kila wiki mbili lakini saa tatu asubuhi ni mapema mno. Ilikubalika kwamba majembe atajadili na bwana Mlamba na kumwambia Elaine muda na tarehe na Elaine atawafahaisha wengine.

Elaine alisema kwamba Bradley alituma barua pepe kuomba radhi kwa kushindwa kusaidia msafara kama alivyoahidi mwezi wa nne. Jax alisema ataandika barua ya malalamiko kwa ITDP kwa jinsi tulivyotendewa na wajumbe walimuunga mkono kufanya hivyo.

**Ofisi**

Jumatatu iliyopita Juma na Elaine walitoa Tsh 60,000 kutoka benki na pamoja na Tsh 10,000 iliyochangwa wiki mbili zilizopita na kumpa Ally Saidi Mohammed ili kununua vifaa vya kutengeneza samani za ofisi. Ofisi yetu / kituo cha maelezo kwa sasa ina mbao tatu za matangazo zilizotengenezwa na Ally Saidi Mohammed. Anaendelea kutengeneza rafu ya magazeti.

**Guta**

Jumatatu Jumanne Eline pia walitoa Tsh 280,000 ili kununua Guta ambalo Mhe Ngaja alikubali kutupunguzia bei. Jumanne Jumanne na Juma walikwenda keko na kununua guta. Jumanne alisema waliomba kupewa rimu na taizi imara za nyuma ili kuepuka tatizo baadae ila hiyo itagharimu Tsh 70,000 zaidi hivyo aliamua kuchukua kwa gharama ya mwanzo. Hata hivyo alisema itatakiwa kufanyiwa ukarabati mkubwa ikiwemo kununua tairi na mipira ambayo itagharimu Tsh 17,000 kuna Tsh 25,000 za mchango kutoka IBike bado ziko kwenye akaunti yetu hivyo ilikubalika kuwa apewe Jumanne ili kununua spea zitakazohitajika na kukamilisha ukarabati.

Ilijadiliwa kuhusu jinsi ya kufanya usimamizi wa guta. Ilikubalika kuwa Jumanne atasimamia kila siku. Bwana Saidi Hemed Mbaruku atakuwa dereva wa guta na atafanya kazi hiyo, kila siku. Atatakiwa kumpa Jumanne Tsh 1,500 kila siku (kama kodi ya kukodisha guta) na kubaki na nyingine. Jumanne ataweka Tsh 500 kwa siku kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya guta n.k. atafanya uangalizi bure. Jumanne atampa Juma Tsha 1000 kila siku (7,000 kwa wiki, kila jumamosi) ili aziweke kwenye akaunti ya UWABA. Fedha hizi zitakusanywa ili kukulipia kodi na matumizi mengine ya ofisi ya UWABA. Sosthenes alisema tunatakiwa kumwamini Jumanne kwani ni mjuzi wa kazi za guta na ni yeye pekee anayeweza kusimamia na kukarabati guta. Juma alikuwa na tatizo kuhusu jinsi usimamizi utakavyokuwa lakini baadae alikubali na kuridhika. Juma alitaka kutafuta dereva mwingine wa guta lakini alikubalika kuwa kwa vile jumanne ndiye atakayesimamia basi yeye ndie achague dereva (Saidi Mbaruku ambaye anamwamini na kumfahamu. Mohamed mwenguo alisema kwamba mfumo huu uandikwe na Elaine alisema ataelezea kwenye dondoo za mkutano.

**Mradi wa upandaji baiskeli salama / wamba memorial Fund**
Jumatatu Elaine na Paulo walikutana na HUWATA katika ofisi yao Ilala wakiandika pendekezo la mradi kwa wamba Memorial Fund kuomba mradi huo. Pendekezo liliandikwa kwa kiingereza hivyo alitafsiri kwa Kiswahili na kuipitisha kwa wajumbe.

Sosthenes alisema kwamba tutafute ukumbi tukaopewa bure badala ya kulipa wakati wa mafunzo. Alisema pia tunatakiwa tuwe karibu na VETA na NIT (chuo cha Taifa cha usafirishaji ambao wanafundisha madereva. Kwa upande wa mradi tunaweza kuongea na wanaofundisha nap engine tukapata ukumbi bure.

Kukamilisha barua ya maombi tunahitaji barua ya utambulisho kutoka serikali za mitaa. Tuliandaa barua kwa serikali za mitaa mtaa wa jitegemee kwa usaidizi wa Mohamed Mwenguo aliyesema atafuatilia jumatatu. HUWATA pia wanafuatilia barua ya utambulisho ambayo wamesema wataipata jumatatu.

**Chuo cha usafirishaji cha Taifa**
Elaine alimpigia bwana Wemba simu wa NIT kumwomba ahudhurie kwenye mkutano, alikubali lakini hakufika. Alimpigia wakati wa mkutano akaahidi kuja wiki ijayo. Jumamosi.

**Sanduku la barua**
Elaine na Juma walitoa Tsh 35,000 kutoka benki siku ya jumatatu, ili kufungua sanduku la posta kwa ajili ya UWABA S. L. P ni 90361,Dar es Salaam.

Juma  pia alitoa nakala ya funguo wa S.L.P la Meja, toka kwa kaka yake Meja. Atajaribisha nakala hiyo na kurudisha ufunguo halisi siku ya jumatatu.

**TANROADS**
Jumatatu asubuhi Juma, Paulo na Elaine walikwenda TANROAD kukutana na bwana NItti kama ilivyopangwa. Tuliambiwa turudi baadae kwani bwana Nitti alikwenda kwenye mkutano Tuliporudi tuliambiwa hawezi kukutana na sisi kabisa. Katibu wa mkurugenzi mtendaji aliomba radhi na kueleza kwamba kulikuwa na tatizo siku hiyo hivyo labda tujaribu wiki ijayo ili tupange kukutana tena.

**Vitambulisho**
Kwa sasa vitambulisho vyetu vina tovuti tu kwa mawasiliano, hivyo Sosthenes alipendekeza kwamba tuweke namba ya simu S.L.P na mahali ilipo ofisi. Elaine alisema kwamba S.L.P na ofisi ni wazo zuri lakini hatuna namba ya simu ya ofisi wa wajumbe wa kamati pengine hawatapenda namba zao kuwa kwenye kitambulisho cha kila mtu. Ilikubalika kuweka S.L.P na mahali ilipo ofisi kwa vitambulisho vitakavyotolewa.

Sosthenes pia alipendekeza kwamba vitambulisho view na picha ya guta na baiskeli ya walemavu pamoja na baiskeli ya kawaida kuakisi UWABA. Kama nembo yetu ilivyo na picha ya baiskeli, ilikubalika kwamba vitambulisho view na picha mbili ndogo za baiskeli ya guta na ya walemavu. Sosthenes alisema atachora picha hizo.